# Ecc

## Chapter 10

### Swahili Interlinear

Reference: Swahili Biblica Neno

1

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| זְבוּבֵי | Nzi-wa | H2070 |
| מָוֶת | mauti | H4194 |
| יַבְאִישׁ | huleta-uvundo | H0887 |
| יַבִּיעַ | na-uharibifu | H5042 |
| שֶׁמֶן | mafuta-ya | H8081 |
| רוֹקֵחַ | manukato | H7543 |
| יָקָר | hivyo-huzidi | H3368 |
| מֵחָכְמָה | hekima | H2451 |
| מִכָּבוֹד | na-heshima | H3519 |
| סִכְלוּת | upumbavu | |
| מְעָט׃ | kidogo | H4592 |

> Kama vile nzi waliokufa huacha harufu mbaya kwenye manukato, ndivyo upumbavu kidogo huzidi nguvu hekima na heshima.

2

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| לֵב | Moyo-wa | |
| חָכָם | mwenye-hekima | H2450 |
| לִימִינוֹ | kulia-kwake | H3225 |
| וְלֵב | lakini-moyo-wa | |
| כְּסִיל | mpumbavu | H3684 |
| לִשְׂמֹאלוֹ׃ | kushoto-kwake | H8040 |

> Moyo wa mwenye hekima huelekea kuume, lakini moyo wa mpumbavu huelekea kushoto.

3

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| וְגַם־ | Na-hata | H1571 |
| בַּדֶּרֶךְ | njiani | H1870 |
| [כשהסכל] | [mpumbavu] | H5530 |
| (כְּשֶׁסָּכָל) | mpumbavu | H5530 |
| הֹלֵךְ | anapotembea | H1980 |
| לִבּוֹ | moyo-wake | |
| חָסֵר | unapunguka | H2638 |
| וְאָמַר | na-anasema | H0559 |
| לַכֹּל | kwa-wote | H3605 |
| סָכָל | mpumbavu | H5530 |
| הוּא׃ | yeye | H1931 |

> Hata anapotembea barabarani, mpumbavu hukosa ufahamu na kudhihirisha kwa kila mmoja jinsi alivyo mpumbavu.

4

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| אִם־ | Kama | |
| רוּחַ | roho-ya | H7307 |
| הַמּוֹשֵׁל | mtawala | H4910 |
| תַּעֲלֶה | inapanda | H5927 |
| עָלֶיךָ | dhidi-yako | |
| מְקוֹמְךָ | mahali-pako | H4725 |
| אַל־ | usiache | H0408 |
| תַּנַּח | kuacha | H3240 |
| כִּי | kwa-maana | |
| מַרְפֵּא | utulivu | H4832 |
| יַנִּיחַ | hutuliza | H3240 |
| חֲטָאִים | makosa | H2399 |
| גְּדוֹלִים׃ | makubwa | |

> Kama hasira ya mtawala ikiwaka dhidi yako, usiache mahali pako, utulivu huweza kuzuia makosa mengi.

5

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| יֵשׁ | Kuna | H3426 |
| רָעָה | uovu | |
| רָאִיתִי | niliouona | H7200 |
| תַּחַת | chini-ya | H8478 |
| הַשָּׁמֶשׁ | jua | H8121 |
| כִּשְׁגָגָה | kama-kosa | H7684 |
| שֶׁיֹּצָא | linalotoka | H3318 |
| מִלִּפְנֵי | mbele-ya | H6440 |
| הַשַּׁלִּיט׃ | mtawala | H7989 |

> Kuna ubaya niliouona chini ya jua, aina ya kosa litokalo kwa mtawala:

6

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| נִתַּן | Amewekwa | H5414 |
| הַסֶּכֶל | ujinga | H5529 |
| בַּמְּרוֹמִים | katika-nafasi-za-juu | H4791 |
| רַבִּים | nyingi | |
| וַעֲשִׁירִים | na-matajiri | H6223 |
| בַּשֵּׁפֶל | katika-nafasi-za-chini | H8216 |
| יֵשֵׁבוּ׃ | wanakaa | H3427 |

> Wapumbavu kuwekwa kwenye nafasi nyingi za juu, wakati matajiri hushika nafasi za chini.

7 רָאִיתִי Nimewaona H7200 | עֲבָדִים watumwa H5650 | עַל־ juu–ya | סוּסִים farasi | וְשָׂרִים na–wakuu H8269 | הֹלְכִים wakitembea H1980 | כַּעֲבָדִים kama–watumwa H5650 | עַל־ juu–ya | הָאָרֶץ׃ nchi H0776

Mimi nimeona watumwa wamepanda farasi, wakati wakuu wakitembea kwa miguu kama watumwa.

8 חֹפֵר Anayechimba H2658 | גּוּמָּץ shimo H1475 | בּוֹ ndani–yake | יִפּוֹל ataanguka H5307 | וּפֹרֵץ na–anayebomoa H6555 | גָּדֵר ukuta H1447 | יִשְּׁכֶנּוּ ataumwa | נָחָשׁ׃ nyoka H5175

Yeye achimbaye shimo aweza kutumbukia ndani yake, yeyote abomoaye ukuta anaweza kuumwa na nyoka.

9 מַסִּיעַ Anayeondoa H5265 | אֲבָנִים mawe H0068 | יֵעָצֵב atajeruhiwa | בָּהֶם nayo | בּוֹקֵעַ na–anayekata H1234 | עֵצִים magogo H6086 | יִסָּכֶן atahatarisha | בָּם׃ nayo

Yeyote apasuaye mawe inawezekana yakamuumiza, yeyote apasuaye magogo inawezekana yakamuumiza.

10 אִם־ Kama | קֵהָה imezimika H6949 | הַבַּרְזֶל chuma H1270 | וְהוּא na–yeye H1931 | לֹא־ hajanoa H3808 | פָנִים kunoa H6440 | קִלְקַל ncha H7043 | וַחֲיָלִים nguvu–zaidi H2428 | יְגַבֵּר zitahitajika H1396 | וְיִתְרוֹן lakini–faida–ya H3504 | הַכְשֵׁר(הכשיר*הַכְשֵׁר) mafanikio H3787 | חָכְמָה׃ ni–hekima H2451

Kama shoka ni butu na halikunolewa, nguvu nyingi zinahitajika, lakini ustadi utaleta mafanikio.

11 אִם־ Kama | יִשֹּׁךְ akiuma | הַנָּחָשׁ nyoka H5175 | בְּלוֹא־ bila H3808 | לָחַשׁ uchawi H3908 | וְאֵין hakuna H0369 | יִתְרוֹן faida H3504 | לְבַעַל kwa–mwenye H1167 | הַלָּשׁוֹן׃ ulimi H3956

Kama nyoka akiuma kabla ya kufanyiwa uaguzi, mwaguzi hatahitajika tena.

12 דִּבְרֵי Maneno–ya H1697 | פִי־ kinywa–cha H6310 | חָכָם mwenye–hekima H2450 | חֵן yana–neema H2580 | וְשִׂפְתוֹת lakini–midomo–ya H8193 | כְּסִיל mpumbavu H3684 | תְּבַלְּעֶנּוּ׃ inamzamisha H1104

Maneno yatokayo kinywani mwa mtu mwenye hekima yana neema, bali mpumbavu huangamizwa na midomo yake mwenyewe.

13 תְּחִלַּת Mwanzo–wa H8462 | דִּבְרֵי־ maneno–ya H1697 | פִיהוּ kinywa–chake H6310 | סִכְלוּת ni–upumbavu | וְאַחֲרִית na–mwisho–wa H0319 | פִּיהוּ kinywa–chake H6310 | הוֹלֵלוּת ni–wazimu H1948 | רָעָה׃ mbaya

Mwanzoni maneno yake ni upumbavu, mwishoni ni wazimu mbaya,

14

| וְהַסָּכָל | יַרְבֶּה | דְבָרִים | לֹא־ | יֵדַע | הָאָדָם | מַה־ | שֶּׁיִּהְיֶה | וַאֲשֶׁר |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Na-mpumbavu | huongeza | maneno | hajui | kujua | mwanadamu | kipi | kitakachokuwa | na-kipi |
| H5530 | | H1697 | H3808 | H3045 | H0120 | H4100 | H1961 | |

| יִהְיֶה | מֵאַחֲרָיו | מִי | יַגִּיד | לוֹ׃ |
|---|---|---|---|---|
| kitakachokuwa | baada-yake | nani | atakayemwambia | yeye |
| H1961 | | H4310 | H5046 | |

> naye mpumbavu huzidisha maneno. Hakuna yeyote ajuaye linalokuja, ni nani awezaye kueleza ni jambo gani litakalotokea baada yake?

15

| עֲמַל | הַכְּסִילִים | תְּיַגְּעֶנּוּ | אֲשֶׁר | לֹא־ | יָדַע | לָלֶכֶת | אֶל־ | עִיר׃ |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kazi-ya | wapumbavu | inawachosha | kwa-sababu | hawajui | kujua | kwenda | kwenye | mji |
| H5999 | H3684 | H3021 | | H3808 | H3045 | H3212 | H0413 | |

> Kazi ya mpumbavu humchosha mwenyewe, hajui njia iendayo mjini.

16

| אִי־ | לָךְ | אֶרֶץ | שֶׁמַּלְכֵּךְ | נָעַר | וְשָׂרַיִךְ | בַּבֹּקֶר | יֹאכֵלוּ׃ |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ole | wako | nchi | ambayo-mfalme-wako | ni-mtoto | na-wakuu-wako | asubuhi | wanakula |
| H0337 | | H0776 | H4428 | H5288 | H8269 | H1242 | H0398 |

> Ole wako, ee nchi ambayo mfalme wako alikuwa mtumwa na ambayo wakuu wako hufanya karamu asubuhi.

17

| אַשְׁרֵיךְ | אֶרֶץ | שֶׁמַּלְכֵּךְ | בֶּן־ | חוֹרִים | וְשָׂרַיִךְ | בָּעֵת |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Heri | nchi | ambayo-mfalme-wako | ni-mwana-wa | wakuu | na-wakuu-wako | wakati-unaofaa |
| H0835 | H0776 | H4428 | | H2715 | H8269 | H6256 |

| יֹאכֵלוּ | בִּגְבוּרָה | וְלֹא | בַשְּׁתִי׃ |
|---|---|---|---|
| wanakula | kwa-nguvu | na-si | kwa-ulevi |
| H0398 | H1369 | H3808 | H8358 |

> Heri wewe, ee nchi ambayo mfalme wako ni wa uzao wenye kuheshimika na ambayo wakuu wako hula chakula kwa wakati unaofaa: ili kupata nguvu na si kwa ajili ya ulevi.

18

| בַּעֲצַלְתַּיִם | יִמַּךְ | הַמְּקָרֶה | וּבְשִׁפְלוּת | יָדַיִם | יִדְלֹף | הַבָּיִת׃ |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kwa-uvivu | huanguka | paa | na-kwa-uzembe-wa | mikono | hudondoka | nyumba |
| H6103 | H4355 | H4746 | H8220 | H3027 | H1811 | |

> Kama mtu ni mvivu paa la nyumba huinama, kutokana na mikono milegevu, nyumba huvuja.

19

| לִשְׂחוֹק | עֹשִׂים | לֶחֶם | וְיַיִן | יְשַׂמַּח | חַיִּים | וְהַכֶּסֶף | יַעֲנֶה | אֶת־ |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kwa-furaha | wanafanya | chakula | na-divai | hufurahisha | maisha | na-fedha | hujibu | — |
| H7814 | | H3899 | H3196 | H8055 | | H3701 | | H0853 |

| הַכֹּל׃ |
|---|
| yote |
| H3605 |

> Karamu hufanywa kwa ajili ya kicheko, nao mvinyo hufurahisha maisha, lakini fedha ni jawabu la mambo yote.

20

| גַּם | בְּמַדָּעֲךָ | מֶלֶךְ | אַל־ | תְּקַלֵּל | וּבְחַדְרֵי |
|---|---|---|---|---|---|
| Hata | katika-mawazo-yako | mfalme | usimlaani | kumlaani | na-katika-vyumba-vya |
| H1571 | H4093 | H4428 | H0408 | H7043 | H2315 |

| מִשְׁכָּבְךָ | אַל־ | תְּקַלֵּל | עָשִׁיר | כִּי | עוֹף | הַשָּׁמַיִם |
|---|---|---|---|---|---|---|
| chumba-chako-cha-kulala | usimlaani | kumlaani | tajiri | kwa-maana | ndege-wa | mbinguni |
| H4904 | H0408 | H7043 | H6223 | | H5775 | H8064 |

| יוֹלִיךְ | אֶת־ | הַקּוֹל | וּבַעַל | [הכנפים] | (כְּנָפַיִם) | יַגִּיד | דָּבָר׃ |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| atabeba | — | sauti | na-mwenye | [mabawa] | mabawa | ataarifu | jambo |
| H3212 | H0853 | | H1167 | H3671 | H3671 | H5046 | H1697 |

> Usimshutumu mfalme hata ikiwa ni katika mawazo yako, au kumlaani tajiri katika chumba chako cha kulala, kwa sababu ndege wa angani wanaweza kuchukua maneno yako, naye ndege anayeruka anaweza kutoa taarifa ya yale uliyosema.